Toleo la: 0072014

TIMER NATIONAL SERIES
EVALUATION TEST
DARASA LA NNE KISWAHILI

{ 4 }

Muda: Saa 1 dakika 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu cha maswali na karatasi ya kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINA LAKO **JINA LA SHULE YAKO**

Jaza mianya kwa kujibu sahihi kutoka kwa swali la 1 hadi 10.

Hospitali ni mahali __1__ kuwatibu watu __2__ magonjwa mbalimbali. Hospitali __3__ huitwa __4__ au kituo __5__ afya. Daktari na mwuguzi hupatikana __6__ hospitali. __7__ ndio huwatibu wagonjwa. Vyumba vya __8__ wagonjwa huitwa __9__ . Vifaa __10__ hospitalini huwa safi sana.

	A	B	C	D
1.	ya	pa	za	wa
2.	yenye	zenye	wenye	mwenye
3.	dogo	mdogo	kidogo	ndogo
4.	bweni	chekechea	zahanati	nyumba
5.	cha	ya	wa	za
6.	kwa	na	kwenye	ndani
7.	yeye	nyinyi	huyo	wao
8.	kuwalaza	kuwalea	kulia	kuweka
9.	darasa	kodi	wodi	chumba
10.	za	ya	vya	la

Darasa __11__ lina wanafunzi ishirini na __12__ na walimu __13__ . Kila mwalimu huja darasani wakati wa kipindi __14__ na wakati hawana vipindi hupumzika kwenye majilisi __15__ .

11.	yetu	letu	zetu	yao
12.	mbili	miwili	mawili	wawili
13.	sita	wasita	wasaba	nane
14.	yake	zao	chake	chao
15.	zao	yao	wao	kwao

Jibu swali la 16-30 kulingana na maagizo.

16. Kamilisha methali:

Kanga hazai _____

A. ugenini B. shimoni

C. majini D. nyasini

17. Mtu ambaye ana nundu mgongoni huitwa _____

A. kigugumizi B. kibyongo

C. kiziwi D. bubu

18. Taja jina la umbo hili _____



A. moyo

B. roho

C. mapenzi

D. kopa

19. Kanusha sentensi ifuatayo:

Nitakuja _____

A. sikuji B. siji

C. sitaja D. sitakuja

20. Je akisami hii huitwaje? $^1/_6$

A. Subui B. Sudusi

C. Humusi D. Robo

21. Mjukuu wangu ataniita _____

A. mjomba B. babu au nyanya

C. shangazi D. binamu

22. Badala ya kusema mtu anahara tunasema _____

A. anaendesha B. anajifungua

C. anazaa D. anataga

23. Kamilisha kitendawili:

Kila siku hupita njia hiyo hiyo lakini arudipo hatumwoni _____

A. garimoshi B. mto

C. jua D. mvua

24. Shati _____ ni la mjomba.

A. leupe B. jeupe

C. nyeupe D. eupe

25. Samaki _____ alivuliwa na mvuvi _____ leo.

A. huyu, hawa B. hii, huyu

C. hawa, huyu D. huyu, huyu

26. Mtu akikusalimia 'sabalkheri' utamjibu _____

A. masalkheri B. aheri

C. hatujambo D. pia wewe

27. Tumia —angu ipasavyo.

Vikombe _____ ni hivi na vyako ni hivyo.

A. changu B. vyangu

C. viangu D. vyetu

28. Kinda ni mtoto wa _____

A. ndege B. kuku

C. nyoka D. mbwa

39. Naomba mkate _____

A. niukule B. nikule

C. nile D. nikakule

30. Matata alitunulia maembe _____

A. sita B. matisa

C. masita D. masaba

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.

Mfalme Kathimba alipenda mzaha sana. Siku moja wakati wa baridi alitangaza kwamba yule angekubali kutumbukia ndani ya maji ya barafu usiku kucha angempa nusu ya mali yake.

Katika ufalme wake paliishi mvulana mmoja maskini aliyeitwa Musa. Alishangaza watu alipojitumbukiza majini usiku kucha. Alitetemeka na meno yake kugongana. Asubuhi alienda kwa mfalme na kumwambia ampe zawadi yake. Alishangaa kwa sababu alikuwa anasema hivyo kwa mzaha. Ilimbidi ampe Musa zawadi.

31. Ni nani alipenda mzaha?

A. Mfalme B. Maji

C. Musa D. Wanakijiji

32. Mfalme alitangaza____

A. anapenda mzaha.

B. watu watetemeke.

C. kila mtu alale majini.

D. mtu aingie majini mpaka asubuhi.

33. Ni nani alikuwa maskini?

A. Mfalme B. Watu

C. Musa D. Barafu

34. Ni nani alijitokeza kuingia majini?

A. Musa B. Mfalme

C. Watu D. Jirani

35. Kwa nini Musa alijitokeza kuingia majini?

A. Awe mfalme.

B. Kumfurahisha mfalme.

C. Alitaka kutetemeka.

D. Apewe zawadi.

36. Musa aliingia majini kwa muda gani?

A. Saa mbili

B. Mchana wote

C. Jioni

D. Usiku wote

37. Musa alirauka kwenda kwa ____

A. barafu B. jirani

C. mfalme D. maji

38. Mfalme hakutaka kutoa zawadi kwa sababu ____

A. ulikuwa mzaha.

B. hakuamini Musa.

C. Musa hakutetemeka.

D. alikuwa na shingo upande.

39. Musa alikuwa ameendea nini kwa mfalme?

A. Kulala majini B. Zawadi

C. Barafu D. Maji

40. Kifungu hiki kinatueleza ____

A. tuwe na mzaha.

B. tutimize ahadi.

C. tuingie kwa maji.

D. tupewe zawadi.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswli 41-50.

Binti Imani Maliwaza alikuwa msichana mrembo aliyeishi katika nchi kavu iliyokaribiana na jangwa. Alikuwa hana chakula cha kutosha nyumbani. Alikuwa mfugaji wa paka watatu, kasuku watano, mbwa sita, ng'ombe wawili na kobe watano. Alikuwa na mahindi kiasi kidogo sana katika **ghala** lake. Basi aliamua kuwapikia wanyama wake kitoweo cha ugali lakini alipoona kwamba hawajashiba, alikitoa chakula chake alichokitegemea na kuwapa wanyama. Huruma iliyoje?

Hakika, maisha yake na wanyama yalikuwa kama chanda na pete. Siku moja alipokuwa nyumbani na mifugo wake, aliusikia mngurumo wa kushtua kutoka nje ya mlango wa chumba chake.

"Ni mnyama yupi huyu anayenguruma nje?" Binti Imani alijiuliza. Alipofungua mlango, alishangaa kumwona simbabuka mmoja mkubwa. Hapo tu, alianguka na kuzimia kwa sababu ya kuliona jinyama lile hatari ambalo limewaangamiza mifugo wake.

41. Ni wanyama gani waliofugwa kwa wingi wa idadi?
A. Kasuku B. Mbwa
C. Kobe D. Paka

42. Imani alipendana na wanyama wake kama
A. ushati na ngozi
B. usiku na giza
C. shilingi kwa ya pili
D. chanda na pete

43. Mbona Imani hakuwa na chakula cha kutosha nyumbani?
A. Kwa sababu ya ukavu wa nchi iliyokaribiana na jangwa.
B. Alikuwa mfugaji wa wanyama wengi wali kimaliza chakula.
C. Hakuwa mkulima shujaa na mahindi yalikuwa machache.
D. Alikuwa mkulima wa mahindi pekee.

44. Alipogundua kuwa chakula hakitoshi, Imani aliamua kuwapikia wanyama chakula kipi?
A. Pure B. Mchuzi
C. Kitoweo cha sima D. Kitoweo cha kuku

45. Mngurumo uliomshtua Imani ulikuwa wa nini?
A. Gari B. Simba buka
C. Chui D. Shetani

46. Simba alifanya nini baada ya Imani kuanguka na kuzimia?
A. Alimla Imani.
B. Aliwala mifugo wote.
C. Alitorokea porini.
D. Hatujaelezwa.

47. Kutoa chakula ghalani na kuwapikia wanyama kunaonyesha kwamba Imani ni _____
A. karimu B. mchoyo
C. mkono birika D. mpishi

48. "Alikuwa na mahindi kiasi kidogo" Maelezo haya yanamaanisha _____
A. mahindi hayakuwepo kabisa.
B. hakuwa na mahindi yoyote katika ghala.
C. mahindi yalikuwa haba.
D. mahindi huliwa kidogokidogo na wanyama.

49. Ghala pia huitwa _____
A. bohari B. zahanati
C. soko D. ghorofa

50. Kichwa cha habari hii kinafaa kuwa _____
A. Maliwaza mchoyo.
B. Maliwaza mpenzi wa wanyama.
C. Imani na simba.
D. Umuhimu wa simba kwa wanyama.